**Utangulizi**

Makala hii imejikita katika uchanganuzi wa maandishi kuhusu nafasi ya upanuzi wa Kiswahili kinapopewa hadhi ya kuwa lugha ya kufundishia. Lugha ya taifa inapotumiwa katika climu, teknolojia na utawala huwa ni fahari kuu kwa taifa husika. Katika nchi zilizo "huru", lugha inayozungumzwa na wananchi wcngi ndiyo hutumiwa katika climu (kufundishia) ambayo huwawezesha wanafunzi kuwa wabunifu, wagunduzi na huzungumza na niioyo yao pamoja na akili zao. Kila janiiilugha hupendclea kuona lugha yake ikikua na kuenea kutoka hatua moja hadi nyingine (kitaifa hadi kimataifa). Kuna ukuniba mkubwa kati ya lugha, elimu. saikolojia na sosiolojia. Kielimu mwanafunzi hujifunza haraka kupitia lugha anayoielewa vyema kuliko lugha ngeni. Kisaikolojia luglta za asili ni mfumo wa alama zenye maana ambazo katika akili ya mwanafunzi hufanya kazi haraka katika kujieleza na kuelewa. Kisosiolojia lugha ya asili ya mtu ni njia ya kujinasibisha na jamii yake. Matokeo ya uchanganuzi wa makala hii inaonyesha kwamba miongoni mwa lugha za kimataifa, Kiswahili kina hadhi ya nafasi ya sita. Aidha, Katika Afrika Mashariki Kiswahili huzungumzwa na takribani watu milioni 100. Kwa hivyo Kiswahili ni lugha ya asili ya wananchi wa Afrika Mashariki. Uteuzi wa lugha ya Kiswahili kufundishia katika viwango vyote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kutaipa lugha hii jukumu na mfumo wake wa kiisimu utapanuka ili kukidhi haja za mawasiliano ya kitaaluma.